WAJA SPRINGS SCHOOLS

WAJA BOYS SECONDARY SCHOOL

P.O Box 561 Geita Mobile: +255 769 218 220/ +255 655 800 052/ +255 756 140 887/ +255 756 141 522

Email: wajaboys@ajageneral**.com**

PASSPORT SIZE

ADMISSION NO:_____ **ADMISSION DATE**:_____

JOINING INSTRUCTION FOR FORM ONE - 2019

STUDENT'S NAME/ JINA LA MWANAFUNZI : _____

GENDER/JINSIA :_____ AGE/UMRI :_____ .

SUBJECT AVERAGE AND GRADE OBTAINED IN STANDARD SEVEN /WASTANI WA UFAULU NA GREDI ALIYOPATA DARASA LA SABA: _____

PSLE NO :_____

PARENT'S /GUARDIAN'S NAME/JINA LA MZAZI /MLEZI :_____

CELL PHONE/SIMU :_____

OCCUPATION /NAFASI YA KAZI :_____

NATIONALITY/URAIA :_____

DISTRICT /WILAYA :_____

APPLICATION FOR FORM: _____

DATE: _____ SIGNATURE: _____

IN CASE OF EMERGENCY/ Ikiwa mzazi haupatikani mtu/ watu wa kuwasiliana nao pindi tunapokuwa na shida:

OTHER CONTACT/MAWASILIANO: _____

NAME/JINA: _____

RELATION TO CHILD/UHUSIANO:_____

NAME/JINA: _____

RELATION TO CHILD/ UHUSIANO: _____

CELL PHONE/SIMU: _____

LOCATION/ MTAA: _____

OFFICIAL USE

HEAD TEACHER'S NAME: _____

DATE: _____ SIGNATURE: _____

APPLICATION FORM REQUIREMENTS:

i) Copy of his/her birth certificate:
ii) Three recent passport size photos
iii) A medical report.

_____

Official Stamp

WAJA SPRINGS SCHOOLS
WAJA BOYS SECONDARY SCHOOL
P.O Box 561 Geita Mobile: +255 769 218 220/ +255 655 800 052/ +255 756 140 887/ +255 756 141 522
Email: Info @ Wajageneral./Chacha@Wajageneral.Com/Jacqueline @Wajageneral.Com

Ndugu……

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA**

Tunapenda kukutaarifu kwamba, ombi lako la kujiunga na shule ya sekondari ya wavulana ya Waja kidato cha …… Mwanafunzi amekubaliwa kwa mwaka wa masomo ……

Tunakuhakikishia elimu bora inayoambana na misingi ya kiroho, kinidhamu, kimaarifa itakayomjenga mtoto kimawazo na kifikra.

Shule ipo Mwatulole km 6 kutoka Geita mjini. Mazingira ya shule ni mazuri kwa ajili ya kusoma na kujifunzia. Shule ina walimu wenye taaluma waliobobea katika kufundisha masomo yao. Hivyo mwanafunzi anayetegemea kujiunga na shule hii, atategemea elimu iliyo bora katika maisha yake ya baadae.

Vigezo vya chini kwa mwanafunzi kujiunga na shule ya Sekondari ya wavulana Waja kwa kidato cha kwanza awe na cheti cha kuhitimu elimu ya msingi.

USAJILI

Uchaguzi wa shule ya kumpeleka mtoto sio jambo rahisi, ni uamuzi wenye manufaa kwa familia na mwanafunzi kwa ujumla.Kwa jinsi hiyo Waja Sekondary ndio suluhisho pekee kwa mafanikio yako na mwanao.

NB: Wastani wa kuvuka /kuingia darasa jingine ni asilimia 60.

SARE YA SHULE:

Mwanafunzi anapaswa kuwa msafi na kuvaa sare ya shule kwa muda wote anapokuwa shuleni.

Kwa hapa shuleni Waja, kuna aina tatu za sare ya shule; ambazo ni

1.Sare ya darasani (huvaliwa jumatatu hadi Ijumaa)

2.Sare ya michezo (huvaliwa wakati wa michezo kila wiki.

3.Sare ya jioni (huvaliwa baada ya masomo)

NB:Shule itafunguliwa tarehe **05/01/2019**.

MGAWANYO WA MALIPO YA SHULE KWA O- LEVEL

Vifaa	Muhula wa kwanza	Muhula wa pili	Kwa mwaka	Jumla kuu pale anapoanza
Usajili	**50,000/=**			**50,000/=**
Karo/Ada ya shule	**1,200,000/=**	**900,000/=**	**2,100,000/=**	**2,100,000/=**
Vifaa vya masomo	**50,000/=**	**50,000/=**	**100,000/=**	**100,000/=**
Maktaba	**70,000/=**		**70,000/=**	**70,000/=**
Sare ya shule	**250,000/=**			**250,000/=**
Kompyuta	**25,000/=**	**25,000/=**	**50,000/=**	**50,000/=**
Maabara	**50,000/=**		**50,000/=**	**50,000/=**
Matibabu	**60,000/=**	**60,000/=**	**120,000/=**	**120,000/=**
Kitambulisho cha shule	**10,000/=**			**10,000/=**
Hela ya tahadhari	**40,000/=**			**40,000/=**
Malazi	**120,000/=**		**30,000/=**	**120,000/=**
Kabati la nguo na vitabu	**50,000/=**			**50,000/=**
Kitabu cha matokeo	**15,000/=**			**15,000/=**
Sahani, Kikombe, Kijiko na Ndoo	**15,000/=**			**15,000/=**
Ukarabati wa majengo	**30,000/=**		**30,000/=**	**30,000/=**
Vinywaji	**40,000/=**	**40,000/=**	**80,000/=**	**80,000/=**
Jumla	**2,075,000/=**	**1,075,000/=**	**2,630,000/=**	**3,150,000/=**

MCHANGANUO KATIKA JEDWALI HAPO JUU

Vifaa vinavyolipwa mara moja anapoanza	
Usajili	50,000/=
Sare za shule	250,000/=
Kitambulisho	10,000/=
Hela ya tahadhali	40,000/=
Malazi	120,000/=
Kabati la nguo	50,000/=
Sahani, Kikombe, Kijiko na ndoo	15,000/=

Vifaa vinavyojirudia kwa mwaka	
Karo,/Ada ya shule	2,100,000
Vifaa vya masomo	100,000/=
Maktaba	70,000/=
Maabara	50,000/=
Matibabu	120,000/=
Malazi	30,000/=
Compyuta	50,000/=
Ukarabati wa majengo	30,000/=
Vinywaji	80,000/=

NB: Malipo yote yafanyike CRDB Bank kwenye Akaunti Namba **0150232274800,** Jina la Akaunti ni **WAJA BOYS SECONDARY SCHOOL**.
Au - Azania Banki kwenye Akaunti namba **012012133350350001** Jina la Akaunti ni **WAJA BOYS SECONDARY SCHOOL.**

-Sare za shule zinapatikana shuleni kwa bei nafuu.
-Wanafunzi wote wanatakiwa kulipia sare za shule.

VIFAA VIFUATAVYO HUTOLEWA SHULENI

Shati 2	24,000/=
Suruali 2	40,000/=
Sweta 1	18,000/=
Soksi (Jozi 2)	16,000/=
Tai 1	5000/=
Vizibao 2	28,000/=
Nguo za michezo (Jozi 2)	40,000/=
Nguo za kushindia (Jozi 2)	80,000/=
Godoro, Mashuka, Chandarua.	120,000/=

VITU MUHIMU VYA KUSAJILIWA

1. Cheti cha kuzaliwa. 2. Taarifa ya mtoto inayotambuliwa na serikali. 3.Risiti ya malipo ya benki ya ada namichango mingine 4.Vifaa vya bweni vinavyohitajika. 5.Picha 3 (passport size)

MAHITAJI MENGINE

6. Viatu vyeusi (pea mbili 2), Kiwi, Brashi ya viatu.
7. Raba nyeupe za michezo na soksi nyeupe pea 2.
8. Track suit ya rangi ya kijivu pea 1
9. Branketi 1
10. Madaftari ya kutosha 11(counter books), Kalamu za wino na risasi za kutosha na Graph pad 1.
11. Kandambili (Malapa)
12 . Taulo, chanuo
13. Pesa ya ziada/kujikimu isiyozidi au kupungua Tsh 50,000/= (Italipwa kwa Mhasibu)
14. Sabuni za kuogea, Kufulia, Mswaki pamoja na dawa ya meno.
15. Mashine ya kunyolea **(WAHIL)**
16. Nguo za kulalia, night dress au Pajama.
17. Bible (wakristo)

WAJA SPRINGS SCHOOLS

WAJA BOYS SECONDARY SCHOOL

P.O Box 561 Geita Mobile: +255 769 218 220/ +255 655 800 052/ +255 756 140 887/ +255 756 141 522

Email: Info @ Wajageneral./Chacha@Wajageneral.Com/Jacqueline @Wajageneral.Com

---

TO: *The Doctor concerned,*

RE: MEDICAL EXAMINATION FORM.

Please examine the following student and furnish me her current health status. Requested by school Authority.

NAME: …….....

ADDRESS:……..
OCCUPATION:…….

1. GENERAL EXAMINATION:

i) Ears:…….....
ii) Eyes:…….
iii) Skin:……
iv) Upper & Lower extremities:…….....
v) Chest:…….....
vi) Abdomen:……...
vii) Dental:……...

2. PAST MEDICAL HISTORY:

3. LABORATORY EXAMINATION:

i) Urinalysis:……
ii) Stool:……
iii) Sputum:……...
iv) B.S:…….
v) Widal Test:…….
vi) U.P.T test:……..

Remarks:

……..

……..

Date:……..

Name:…….. **Title: ……** **Signature: …**……

SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA WAJA
SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

A: MWANAFUNZI AKIFANYA MAKOSA YAFUATAYO ATAFUKUZWA SHULE

1. Wizi wa aina yoyote au unyang'anyi wa aina yoyote .
2. Uasherati, Ubakaji,Ushoga,ulawiti,usagaji,unajisi au uhusiano wowote wa kimapenzi.
3. Ulevi wa pombe ,matumizi ya madawa ya kulevya (bangi, mihadarati n.k) na uvutaji sigara.
4. Kupigana,kupiga,kuua, kujeruhi mtu yeyote au kutenda ukatili wa aina yeyote.
5. Kupata mimba, kutoa mimba,kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
6. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni au nje ya shule.
7. Kugomea adhabu kwa makusudi shuleni.
8. Kumiliki simu, Kutumia simu ya mtu yeyote au kumiliki vifaa vya simu mfano (earphone,charger ya simu, line za simu n.k),.
9. Kufanya mizaha wakati wa ibada au kuvuruga ibada.
10. Kutoroka shuleni.
11. Kumiliki au kutumia vifaa vya umeme mfano: Heater, Pasi, computer n.k , vifaa vya muziki,silaha ya aina yeyote ile au pesa awapo shuleni.
12. kutumia lugha ya matusi,kejeli, kudanganya utawala au kudharau walimu,wafanyakazi wasio walimu au wazazi/walezi.
13. Kuharibu mali za shule mfano, majengo ya shule, samani n.k au mali ya mtu mwingine kwa makusudi
14. Kuandaa,kushiriki,au kuendesha kikao kisicho na idhini ya utawala wa shule.
15. Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa taifa.
16. Kuoa au kuolewa.
17. Kutenda kosa lolote la jinai.

B. MWANAFUNZI AKIFANYA MAKOSA YAFUATAYO ATASIMAMISHWA MASOMO KWA MUDA USIOZIDI SIKU ISHIRINI NA MOJA (21)

1. Kutovaa sare stahiki mahali stahiki (uvaaji wa sare isivyotakiwa au kufanyia marekebisho bila kibali cha ofisi ya nidhamu).
2. Kuonekana kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi bila idhini ya utawala wa shule.
3. Kuvaa, mikufu,bangili au hereni shuleni, kujiremba mfano kupaka wanja, kufuga nywele, ndevu, kuweka dawa nywele,kupaka kucha rangi,kujichora kwenye mwili au kunyoa mtindo usiokubalika shuleni.
4. Kuchelewa kurudi shuleni mara baada ya shule kufunguliwa.
5. Kutopatikana mahali sahihi kwa wakati sahihi kama vile mikusanyiko, michezo,vipindi vya darasani,kwenye ibada n.k
6. Kuongea na mgeni yeyote ndani au nje ya uzio wa shule bila kibali cha mkuu wa shule.
7. Kuagiza/kununua chakula au vinywaji nje ya shule.
8. Kuvaa kofia,viatu vya ghorofa au vyenye urembo wa aina yeyote.
9. Kukutwa na chakula/kinywaji chochote bwenini au darasani isipokuwa maji ya kunywa.

NB: Endapo mwanafunzi atarudia makosa ya sehemu B Atafukuzwa shule moja kwa moja.

C. MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUYAFANYA NA AKIYAKIUKA ATAADHIBIWA KWA MUJIBU WA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.

1. HESHIMA

Mwanafunzi anapaswa

a) Kusalimu walimu/watu wenye umri zaidi yake kwa kusimama.
b) Kuwaheshimu watu wote; walimu,wafanyakazi wasio walimu, wageni wanaotembelea shule, viongozi wa serikali ya wanafunzi na wanafunzi wenzake.
c) Kuheshimu bendera ya taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa, wimbo wa shule, nyimbo za ibada au kengele ya shule.
d) Kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, mali za shule, mali ya umma au mali ya mtu mwingine.
e) Kusimama anapouliza au kujibu swali, lakini pia anyooshe mkono kuonesha ana shida,mchango au mawazo
f) Kuomba ruhusa anapotaka kutoka nje/kuingia darasani.
g) Kuwasiliana na kuongea kwa lugha ya kiingereza muda wote awapo shuleni.

2. MAHUDHURIO

Mwanafunzi anapaswa:

a) Kuhudhuria vipindi vyote vya darasani, michezo, masomo ya asubuhi (morning prep) na ya jioni (evening prep) kufika kwenye makusanyiko (Assembly) kama inavyotakiwa.
b) Kuhudhuria mikutano yote ya shule (darasani,bwenini au school baraza).
c) Kulala sehemu aliyopangiwa na uongozi wa shule na si vinginevyo.
d) Kutopiga kelele bwenini,darasani,maabara,maktaba na sehemu za mikusanyiko.

3. SARE ZA SHULE

Mwanafunzi anapaswa

a) Kuvaa sare za shule kama ilivyokusudiwa
   i. Sare za darasani
   ii. Sare za nje ya darasa
   iii. Sare za michezo
   iv. Sare wakati wa masomo ya jioni (track suits za kijivu)
b) Kuvaa sare zenye heshima <u>zisizobana</u>, <u>zisizo fupi</u>, na <u>zivaliwe kwa staha.</u>
c) Kufua sare za shule kila mara inapotakiwa.
d) Kuvaa sare zake mwenyewe lakini pia hatakiwi<u>kuazima</u> sare kwa mwanafunzi mwingine.
e) Kukaguliwa wakati wowote awapo ndani au nje ya darasa.

4. SAMANI NA MALI ZA SHULE

Mwanafunzi anapaswa

a) Kutunza samani za shule
b) Kuepusha uharibifu wa vifaa mbalimbali vya shule
   LA SIVYO: Mwanafunzi atapaswa kulipa thamani ya samani/kifaa alichokiharibu.
c) Kutumia samani alizopangiwa na shule tu na kuzirudisha mahali alikozitoa mara baada ya matumizi.

5. USAFI

Mwanafunzi anapaswa

a) Kuweka mazingira ya shule, darasa, bweni , mavazi na mwili wake katika hali ya usafi wakati wote.

b) Kutandika kitanda vizuri, kung'arisha viatu vyake ,kutunza vitu vyake vizuri mahali panapo takiwa na kufanya usafi wake binafsi kwenye maeneo husika.
c) Kufanya usafi wa mazingira ya shule kama alivyopangiwa na uongozi wa shule.

NB:Endapo mwanafunzi ATASHINDWA KUFUATA MAELEKEZO ya sehemu C kwa kujirudia mara tatu atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku ishirini na moja

KIAPO

I: MWANAFUNZI

Mimi……nikiwa na akili timamu nimezisoma sheria zote za shule na kuzielewa na niko tayari kuzifuata na endapo nitakiuka uongozi wa shule unichukilie hatua kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za shule.

SAHIHI……..TAREHE……..

II: MZAZI/MLEZI

Mimi ……Mzazi/Mlezi wa.....nimezisoma sheria zote na kuzielewa vizuri, nimeridhia kwa hiari yangu kuwa endapo kijana wangu atakikiuka sheria hizi, basi uongozi wa shule uchukue hatua kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

SAHIHI…….TAREHE…….

WAJA SPRINGS SCHOOLS

BOYS SECONDARY SCHOOL

P.O Box 561 Geita Mobile: +255 769 218 220/ +255 655 800 052/ +255 756 140 887/ +255 756 141 522

Email: Info @ Wajageneral./Chacha@Wajageneral.Com/Jackline @Wajageneral.Com

SHERIA ZA SHULE.

1. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu, vifaa vya muziki, umeme au silaha ya aina yoyote ile akipatikana na kosa hilo atarudishwa nyumbani/ kufukuzwa shule.

2. Kila mwanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya shule kwa wakati.

3. Mwanafunzi asipokuwepo shuleni au katika shughuli zozote za shule ni lazima kuwe na sababu inayoeleweka. Mfano awe na kibali cha mwalimu wa zamu au wa darasa, patron au nesi.

4. Ruhusa ya kutoka nje ya shule wakati ambao sio sa likizo itatolewa na Mkuu wa shule au Makamu wake.

5. Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mgeni yoyote yule nje ya shule kupitia kwenye uzio au kuonekana nje ya geti. Kosa hilo litapelekea kufukuzwa shule.

6. Mwanafunzi akipatikana na kilevi cha aina yoyote ile kama vile: pombe, mihadarati, (madawa ya kulevya) au akiwa amelewa atarudishwa nyumbani moja kwa moja yaani (atafukuzwa shule).

7. Mwanafunzi akipatikana na wizi au aina yoyote atafukuzwa / ataondolewa shuleni moja kwa moja.

8. Mwanafunzi anapaswa awe mahali anapohitajika kwa wakati kama vile mikusanyiko, wakati wa michezo, wakati was ala .n.k.

9. Mwanafunzi anapaswa kuweka mazingira ya shule, darasa la bweni safi muda wote.

10. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na uhusiano wa kimapenzi kwa namna yoyote ile.Kinyume na hapo atarudishwa nyumbani au kufukuzwa shule.

11. Mwanafunzi atapaswa kuheshimu bendera ya Taifa inapopandishwa na kushushwa na wakati wa Kuimba Wimbo wa Taifa.

12. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya shule wakati wowote kulingana na ratiba ya shule, asiifanyie Marekebisho yoyote mfano kuipunguzwa.

13. Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana kwenye nyumba za walimu na wafanyakazi wengine bila ruhusa.

14. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa vito vya thamani, kujiremba, mfano kupaka wanja, kupaka kucha rangi, Kuweka nywele dawa n.k

15. Mwanafunzi anapaswa kufuata ratiba na mihula ya shule kikamilifu mfano kurudi shuleni kwa wakati tarehe za kufungua shule.

16. Mwanafunzi ni lazima apime afya kabla ya kuja shuleni na aje na fomu yenye uthibitisho wa daktari aliyeidhinishwa na serikali.

17. Mwanafunzi anaruhusiwa kutembelewa muda uliopangwa na shule tu.

18.Mwanafunzi anaruhusiwa kutembelewa na mtu anayetambuliwa na shule tu.

19.Mwanafunzi anapaswa kutumia lugha za kiingereza na kifaransa tu pindi awapo shuleni.

20. Mwanafunzi haruhusiwi kugombana, kupigana au kumwonea mwenzake pindi awapo shuleni.

21. Mwanafunzi anapaswa kufuata sheria na kanuni za shule pamoja na kutimiza wajibu wake kikamilifu.

22. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na pesa yeyote awapo shule(pesa za matumizi zikabidhiwe kwa muhasibu).

NB.

Uongozi wa shule una haki ya kubadili sheria wakati wowote.

Iwapo mwanafunzi atarudia kosa mara kwa mara uongozi wa shule unaweza kumsimamisha masomo moja kwa moja.

Baada ya kuzisoma sheria na kuzielewa tafadhali thibitisha kukubaliana nazo kwa kujaza hapa chini.

JINA LA MWANAFUNZI ……..…… SAHIHI …….. TAREHE…….

JINA LA MZAZI ……...…… SAHIHI ……. TAREHE……